## Maswali

1. Nani alilala na akaanguka kutoka kwa dirisha?
2. Nani alimponya Eutiko?
3. Mbona Paulo alikasirika alipowaaga marafiki wake Wakristo?
4. Agapo alifanya Paulo nini na akamwambia nini?
5. Wayahudi walisema Paulo alifanya nini?
6. Nani alimshika Paulo?
7. Mbona Gavana wa Warumi hakuweza kuelewa makosa ya Paulo?
8. Mbona Paulo hakupata uamuzi wa haki?
9. Mungu aliambia Paulo nini?
10. Paulo alitaka kufanya nini?

## Majibu

1. Eutiko aliaanguka kutoka kwa dirisha.
2. Paulo aliamsha Eutiko na akamrudishia uzima.
3. Paulo alijua hatawaona tena.
4. Agapo alifunga mikono na miguu yake pamoja kwa mshipi wa Paulo. Alisema hivyo ndivyo mwenye huu mshipi atafungwa huko Yerusalemu.
5. Walisema kwamba Paulo alikuwa amempeleka Mtaifa ndani ya Hekalu.
6. Gavana wa Kirumi alimshika Paulo.
7. Kila mtu alikuwa anapiga kelele akisema mambo tofauti. Kulikuwa na kelele nyingi.
8. Paulo alikuwa Mrumi. Warumi wote walitakiwa wawe na hukumu ya haki.
9. “Usiogope. Nitakulinda. Utahubiri Rumi.”
10. Paulo alitaka kuhukumiwa akiwa Rumi kwa Kaisari.

# SHULE YA JUMAPILI YA CBM

## Awamu ya 2 Mwaka wa 2

# 100 Paulo anashikwa


### Kwa Biblia

Matendo ya Mitume mlango wa 20 : 7 – 12 na milango ya 21 na 22

### Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu alikuwa karibu na Paulo na alimlinda. Paulo hakuogopa kwa sababu aliamini Mungu

### Somo



Paulo alisafiri kwenda Yerusalemu. Alitaka awe Yerusalemu kwa wakati wa siku kuu ya Pentekoste. Kwa safari yake alitembelea miji mingi. Aliwapa Wakristo wote moyo kwa makanisa yenye alikuwa amefungua. Makanisa mengi walimpa Paulo pesa ili apelekee Wakristo maskini wa Yerusalemu.

Paulo aliendа kuona Wakristo waliokuwa Troa. Paulo alikutana nao ili kumega mkate kama dhabihu ya ukumbusho wa Yesu. Paulo alizungumza na Wakristo kwa muda mrefu mpaka usiku wa manane. Kulikuwa na joto jingi_kwa orofa. Kijana mmoja jina lake Eutiko alikuwa amekaa dirishani. Masaa zilipoendelea huyu kijana alichoka na akalala.



Eutiko alikuwa amelala. Alianguka kutoka dirishani. Alianguka kutoka kwa orofa ya tatu mpaka chini. Hawakumwendea haraka. Eutiko alikuwa amekufa zamani. Paulo aliambia watu wote kwamba wasiwe na wasiwasi. Paulo alimrudishia Eutiko uzima. Kila mtu alimshukuru Paulo. Walikuwa na furaha kwa sababu Eutiko alikuwa mzima tena.

Paulo alitembelea Wakristo wengi alipokuwa safarini akienda Yerusalemu. Hakukuwa na furaha akiwaaga marafiki wake Wakristo. Paulo alijua hatawaona tena. Mungu alikuwa amemwambia anaenda kushikwa kule Yerusalemu. Aliambia Wakristo kwamba hajaogopa kwenda gerezani. Alijua kwamba Mungu atakuwa karibu na yeye. Paulo hakuogopa kufa kwa sababu ya Yesu. Alijua Yesu atamfufua kutoka kwa wafu wakati atarudi hapa duniani.

Paulo alikaa Kaisaria na Wakristo. Nabii Agapo alikuja kuona Paulo. Agapo alichukua mshipi wa Paulo. Akafunga mikono na miguu yake. Akasema, "Roho Mtakatifu anasema kwamba Wayahudi wa Yerusalemu watafunga mwenye huu mshipi. Wayahudi watampeana kwa Mataifa." Paulo hakuogopa. Alijua Mungu ako karibu naye. Mungu atamlinda.


Paulo alifika Yerusalemu. Wakristo walimkaribisha. Paulo aliwambia kwamba Mungu alikuwa amemlinda. Paulo aliwambia kwamba Mataifa walikuwa wameamini Injili na wakabatizwa. Wakristo wa Yerusalemu walifurahi kusikia habari ya Wakristo wengi kwa miji yenye Paulo alienda. Wakristo wa Yerusalemu walimhadharisha Paulo kwamba Wayahudi wamemkasirikia. Wayahudi walijua Paulo alikuwa akihubiria Mataifa. Wayahudi walipanga kumua.

Wayahudi waliona Paulo na Mtaifa Yerusalemu. Waliona Paulo akienda kwa Hekalu. Walifikiri alikuwa ameenda na rafiki wake Mtaifa mpaka Hekaluni. Ilikuwa kinyume na sheria Mtaifa kwenda Hekaluni. Adhabu ilikuwa kifo. Paulo alitii sheria. Hakupeleka rafiki wake Mtaifa ndani ya Hekalu.

Wayahudi walipiga kelele kwamba Paulo alikuwa amepeleka Mtaifa ndani ya Hekalu. Umati ulikusanyika. Watu walikimbia kuona nini ilisababisha kelele. Wayahudi waliendelea kupigia Paulo kelele. Umati ulikuwa na ghadhabu kuu. Waliburura Paulo mpaka nje ya Hekalu. Walikuwa wanajaribu kumua. Mji wote wa Yerusalemu ulikuwa na ghasia.

Jemadari wa Kirumi alisikia makelele. Alichukua askari na akakimbia mpaka kwa huo umati. Umati ulipoona Jemadari wa Kirumi pamoja na askari, waliacha kumpiga Paulo. Huyo Jemadari alishika Paulo. Paulo alifungwa kwa minyororo miwibili.

Huyo Jemadari wa Kirumi alijaribu kujua Paulo tena alifanya nini. Umati ulipiga kelele wakisema mambo tofauti. Jemadari hakuelewa nini ilikuwa imefanyika kwa sababu kulikuwa kelele nyingi na machafuko. Ililasimisha askari wabebe Paulo mpaka ngome ya Kirumi ili umati uwache kumua.



Jemadari hakujua Paulo alikuwa amekosa nini. Paulo alikuwa Mrumi. Warumi wote walitakiwa wawe na hukumu ya haki. Jemadari alitaka ajue ni nini Paulo alikuwa amekosa. Halafu angeamua vile atamwadhibu.

Paulo alipelekwa kwa koti ya Wayahudi. Wayahudi hawakusikisana juu ya kosa gani Paulo alikuwa amefanya. Wayahudi walikasirikia Paulo sana. Wayahudi walikuwa wakali sana. Jemadari aliogopa kwamba Paulo anaweza kuawa. Aliamrisha Paulo arudishwe ndani ya ngome.

Usiku huo, Mungu alizungumza na Paulo akamwambia, "Usiogope. Niko ninakulinda. Umehubiri Yerusalemu. Utahubiri Rumi pia."

Paulo aliwekwa gerezani kwa miaka miwili. Paulo alipelekwa kwenda kuhukumiwa na Gavana wa Kirumi. Lakini hawangeweza kuamua kwa sababu hawakujua makosa ya Paulo. Wayahudi waliendelea kupanga kumumaliza. Walitaka wamuue. Paulo aliambia Gavana wa Kirumi, "Ninataka nihukumiwe na Kaisari." Kwa hivyo alipelekwa Rumi ili ahukumiwe na Kaisari.